

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**

**MKOA WA NJOMBE**

**Simu: 026-2968833**

**Faksi: 026- 298832**

**E- mail: [td@njombetc.go.tz](mailto:td@njombetc.go.tz)**

**[njombetc@gmail.com](mailto:njombetc@gmail.com)**



**S.L.P 577,  
NJOMBE.**

**Tovuti: [www.njombetc.go.tz](http://www.njombetc.go.tz)**

**TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa maandalizi ya mashindano ya usafi na mazingira kitaifa yameanza rasmi katika ngazi za Halmashauri kote nchini.

Kuanzia tarehe 30/05/2017 Halmashauri ya Mji Njombe inataraji kupokea ugeni wa kitaifa unaohusiana na maswala ya usafi na mazingira lengo ikiwa ni kufanya ukaguzi na kutembelea maeneo ya Halmashauri na kujionea ni kwa jinsi gani shughuli za usafi zinavyoendeshwa kuanzia ngazi ya Kaya, maeneo ya biashara ,masoko na kuona jinsi gani Halmashauri inashiriki katika kudhibiti taka toka eneo la uzalishaji mpaka eneo la dampo kuu.

Kwa kuzingatia umuhimu wa mashindano hayo ambapo Halmashauri yetu imekua ikifanya vizuri kwa vipindi vyote na kuibuka washindi wa zawadi mbalimbali na kwa kutambua umuhimu wa usafi katika kuepuka magonjwa yanayoambukiza kama kipindupindu na magonjwa ya kuhara,

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anatoa rai kwa wananchi wote kuhakikisha wanaweka mazingira yao safi wakati wowote kwa kufanya yafuatayo;

- Kufanya usafi katika maeneo yao ya kuishi na maeneo ya biashara
- Kuhakikisha kuwa maeneo ya biashara na mabasi ya abiria yanakua na Vifaa maalumu vya kutunzia taka (Dustbin)
- Taka zote zinazozalishwa ziifadhiwe vizuri na kutolewa pindi magari ya taka yanapopita yaweze kukusanya na kupeleka dampo kuu kwa kufuata ratiba iliyopo
- Kuepuka utupaji taka ovyo zikiwemo chupa za maji na karatasi katika maeneo mitaro, maeneo ya wazi na badala yake kutunza taka na kuzihifadhi kwenye vyombo maalumu vya kuhifadhi taka
- Kuhakikisha kuwa migahawa inakuwa katika hali ya usafi na watumishi wawe na sare na kuwa na maji ya moto wakati wote.

- Kuhakikisha wananchi wote kutotiririsha/kumwaga maji machafu kwenye mitaro na kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

***“Kipindupindu Kwetu ni Mwiko, Ushindi ni Lazima. Mimi na Wewe tushirikiane kuweka maeneo yetu safi kila sekunde”***

***Imetolewa Na,  
Afisa Habari  
Halmashauri ya Mji Njombe.***